# The Berean

AFRICA

**Mwili wa Kristo barani Afrika na ulimwenguni unapaswa kuwa mwili unaolenga kuelimisha na kutia moyo kupitia katika maandiko.**

JUZ 16 , APR



...walilipokea neno kwa moyo ulio tayari kabisa, na kuyachunguza maandiko kila siku, kama mambo hayo yalikuwa kweli."

KRISTO ANAKUJA HIVI KARIBUNI NA ATATAWALA DUNIANI

Toleo la 016

# Kutuhusu WABEROYA

## Kristadelfiani



### Masomo ya Aprili

- Hesabu
- Kumbukumbu la torati
- Mhubiri
- Luka
- Wagalatia
- Waefeso
- Wafilipi
- Yohana
- Matendo ya Mitume



### Vikundi vya Kusoma Biblia


Hebu tusome Biblia mtandaoni pamoja.Tuna vikundi mbalimbali vya kusoma Biblia vinavyofaa kwa kila mmoja wetu.Tukisoma Biblia pamoja kwenye WhatsApp, Zoom na katika mikutano yetu, tunajifunza kutoka kwa kila mmoja wetu.



### Ushirika Wetu? Tuulize Chochote

nnalolile@bereanchristadelphian.africa





### Eklezia Zetu Duniani

Ahsante kwa Kazi kwa Eklezia zilizopo Kenya, Malawi, Zambia, Uganda, Tanzania, Marekani, Kanada, Msumbiji, Australia na Papua New Guinea.

Matendo 17:10 — Waberoya walikuwa waungwana zaidi kuliko watu wa Thesalonike, kwa maana walilisikiliza neno la Mungu kwa hamu wakachambua maandiko kila siku ili waone kama waliyokuwa wakiambiwa na Paulo ni kweli.

# KUJISALIMISHA KWA MUNGU




**Mithali 11:17**

Hii inahusisha kumfanya Mungu kuwa kipaumbele chetu cha kwanza, kujisalmisha kwa Utawala Wake na kuoanisha vitendovyetu vya kila siku na kanuni za kibiblia badala ya tamaa za kibinafsi/matamanio ya kidunia..

Ingawa ni mchakato wa mpito kutoka kujitegemea hadi kumtegemea Mungu, tunapaswa kuishi kama dhabihu zilizo haiili kutumiwa kwa madhumuni Yake, tukizingatia mambo yafuatayo:

1. **Kusoma Maandiko/Biblia kila siku.**

Inapaswa kuwa tabia binafsi kujua ahadi za Mungu na amri zake kwetu. Si kusoma tubali kutumia yale tunayojifunza katika vitendo vyetu vya kila siku kwani vitendo vinazungumza zaidi kuliko manenokama inavyoonyeshwa katika Yakobo 2:17. Kwa kufanya hivyo, tunalindwa dhidi ya majaribu.

**2. Kumwogopa na kumwabudu Mungu.**

ChaguakumtukuzaMunguhatakatikahalingumuzaidi, ukitambuakwambamaumivuyanawezakukuleta karibu zaidi naye na kukusaidia kukua kiroho.

3.**Kumtumikia na kumpenda.**

Kwa kuwa hii ni mojawapo ya amri kuu; kumpenda Mungu wetu kwa moyo wetu wote, nafsi yetu yote na akili na zaidi ya yote kupenda jirani zetu kwa moyo wote bila kutarajia thawabu yoyote—Mathayo 22:36-40.Ni wajibu wetu kuonyesha upendo, 1 Wakorintho 13:1-10.

- Hebu tutumie vipawa tulivyopewa na Mungu kwa madhumuni Yake, si kwa faida ya kibinafsi tu.
- Tunapowakosea wengine tunaombwa kukubali makosa yetu kila wakati na dhambi zetu kwa Mungu,tukiruhusu neema Yake kuturejesha badala ya kuruhusu hatia ituondoe kwake.

Dada Ketray - Kabusasi Ecclesia



# Imani Inayotegemewa

Ni wazi basi kwamba tunahitaji mamlaka ya kuaminika na yasiyobadilika ambayo tunaweza kujenga imani zetu juuyake;mamlaka ambayo tunaweza kuiamini kabisa na inayotufanya tujue hasa mahali tulipo na tunachotarajia kwa siku zijazo.Tunahitaji imani inayoweza kutusaidia kupita katika hali zote mbalimbali za maisha bila kutupa sababu ya kutia shaka.

Je, mamlaka kama hiyo ipo?
Ndiyo!
Katika mfumo wa Biblia, neno la Mungu. Fikiria kile inachosema kuhusu umuhimu wa kuamini kile ambacho Munguametangaza kuwa ya kweli, badala ya yale ambayo mwanadamu anafikiri ni sahihi:

"Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu, lakini mwisho wake ni njia za mauti." **Mithali 14:12**

"Mtu aikosaye njia ya busara Atakaa katika mkutano wao waliokufa." **Mithali 21:16**

"Kila neno la Mungu limehakikishwa; Yeye ni ngao yao wamwaminio.Usiongeze neno katika maneno Yake; Asije akakulaumu, ukaonekane u mwongo."**Mithali 30:5-6**

"Na waende kwa sheria na ushuhuda: ikiwa hawasemi sawasawa na neno hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi."**Isaya 8:20**

Biblia inaweka wazi kwamba ufahamu wetu juu yake lazima uwe sahihi ikiwa tunataka kufaidika na tumaini inalofunua.
Hakuna nafasi kwa mwanadamu kuitafsiri upya kulingana na anavyoona yeye mwenyewe,kile ambacho jamii inahitaji. Kama Mungu mwenyewe anavyotangaza:
"Kwa maana mimi ni BWANA, sibadiliki..."**Malachi 3:6**

Ndugu.
Evans Odira.

Mikutano ya Eklezia ya Afrika Mashariki

APR
026







# MKUTANO WA KILA MWAKA WA APRILI









# Eklezia ya Waberoya ya Afrika

Habari na Matukio

**Mkutano Mkuu wa Afrika wa Desemba 2026 wa Ndugu wa Beroya Kristadelfiani**

Eneo: **Busia/Madowa**, **Uganda**
Tarehe: 17 - 20 Desemba, 2026

Kauli mbiu: Mgeuzwe

**Mkutano wa Vijana wa Kusoma Biblia.**

Eneo: **Chitwanga Ecclesia, Malawi**

Tarehe: **Mei 26-28, 2026.**

# Eklezia ya Beroya za Afrika

Habari na Matukio

**Tangazo Muhimu kuhusu Matumizi ya SHA Hospitalini**

**Ndugu na dada,**

**Tafadhali thibitisha na kila hospitali kabla ya matibabu iwapo imeidhinishwa na SHA. Serikali imeondoa ufadhili wa SHA katika baadhi ya hospitali.**

**Pia kumbuka kwamba hospitali zina mipaka tofauti ya gharama z matibabu. Kama matibabu yako yanapita kikomo, utahitaji kulipa kiasi cha ziada kama nyongeza.**

**Tafadhali tuma mawasiliano ya eklezia za kiafrika kwa:**

Timu ya Uhariri
nnalolile@bereanchristadelphian.africa

Akisaidiwa na
Bro. David Mutia
P.O BOX 1, KITUI
study@bereanchristadelphian.africa



**Itaendelea mwezi ujao ijazo ikiwa Bwana atapenda.**